# MWONGOZO MUHIMU wa Masuala ya Kisheria Kuhusu Kilimo Biashara





LIMAS

LINDI AND MTWARA AGRIBUSINESS SUPPORT

# MWONGOZO MUHIMU wa Masuala ya Kisheria Kuhusu Kilimo Biashara

Toleo la pili lililoboreshwa (Novemba 2015)

**MRADI WA KUSAIDIA KILIMO BIASHARA LINDI NA MTWARA**

LIMAS

LINDI AND MTWARA AGRIBUSINESS SUPPORT

JAMANA Printers, Dar es-Salaam, January 2016

# Utangulizi

Urasimishaji wa biashara unajumuisha masuala kadhaa ya kisheria ambayo sharti yazingatiwe wakati wa kuanzisha na kuendeleza biashara. Baadhi ya masharti hayo ni ya lazima kwa biashara zote na mengine yanahusu aina fulani za biashara. Masuala ya urasimishaji yanahusisha, pamoja na mambo mengine, usajili wa biashara katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); kufahamu taratibu za kodi za biashara kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Ofisi za Biashara katika Halmashauri za Wilaya; umiliki wa ardhi; ithibati ya usindikaji chakula na viwango vya usalama na ubora kutoka kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Shirika la Viwango (TBS), na taratibu zinazohusu uhifadhi mazao katika maghala.

Kijitabu hiki kilichapishwa kwa mara ya kwanza mwezi Juni 2015. Hili ni toleo la pili la kijitabu lililoboreshwa, na umeandaliwa na Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED) ya Dar es Salaam, kwa kushirikiana na Mradi wa Kusaidia Kilimo Biashara Lindi na Mtwara (LIMAS), kwa ufadhili wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Finland.

Mwongozo huu umetoa angalizo pale ambapo sheria au kanuni inatofautiana na hali halisi au utekelezaji wa kila siku wa kanuni hizo. Hata hivyo, ieleweke kuwa Mwongozo huu si mbadala wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na mamlaka husika.

LIMAS imechukua tahadhari zote kuhakikisha kuwa hakuna makosa ya tafsiri au uchapaji na hivyo haitahusika na makosa yoyote yatakayobainika.

Ripoti kamili ya kijitabu hiki kinapatikana kwenye **www.limas.or.tz**

# Yaliyomo


Utangulizi ..... 3

**1. Usajili wa Biashara ..... 6**

**2. Kodi/Tozo na Michango ..... 10**

2.1 Kodi ya Mapato ..... 10

2.2 Kodi ya Makampuni ..... 13

2.3 Kodi ya majengo ..... 13

2.4 Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ..... 13

2.5 Kodi ya huduma ..... 13

2.6 Kodi ya mandeleo ya ufundi TRA ..... 13

2.7 Kodi ya zuio ..... 13

2.8 Ushuru wa soko ..... 14

2.9 Ushuru wa mazao wa serikali za mitaa ..... 14

**3. Viwango vya Ubora vinavyo-husiana na Usindikaji na uuzaji wa vyakula ..... 15**

3.1 Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) ..... 15

3.2 Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ..... 15

**4. Usajili wa Maghala ..... 16**

**5. Usajili wa Vyombo vya Usafirishaji ..... 16**

**6. Masuala Mengine ya Kisheria Kilimo ..... 17**

6.1 Kilimo cha Mkataba ..... 17

6.2 Pembejeo za Kilimo ..... 17

6.3 Vibali vya Usafirishaji Mazao na Mifugo ..... 17

6.4 Wakala wa Vipimo (WMA) ..... 17

6.5 Mahitaji ya ufungshaji wa bidhaa kwa mujibu wa Wakala Wa Vipimo ..... 18

6.6 Vikwazo vya Biashara visivyo vya Ushuru (NTB) ..... 18

6.7 Sheria za Kazi ..... 18



**MWONGOZO RAHISI** booklet is based on a study report **"Survey of Key Legislative Issues Related to Agribusiness"**. The study was done by Institute of Management and Entrepreneurship Development (IMED) in October 2014, commissioned by Lindi and Mtwara Agribusiness Support Project LIMAS, P.O.Box 113, Mtwara. Quality assurange for the first edition was done by Claritas International (www.claritas.co.tz).

**This is the second, fully revised edition of the booklet**, based on the information available in November 2015. As regulations are frequently updated the reader is advised to refer to the respective authoirities and entities for possible updates. The publisher will not be liable of inconveniences potentially caused when using the information in this publication.

The production of the booklet has been facilitated by LIMAS, a bilateral development project that is funded jointly by the Governments of Tanzania and Finland. LIMAS is being implemented in Mtwara and Lindi regions in 2011 – 2016.

MWONGOZO RAHISI can be downloaded free of charge at **www.limas.or.tz**

# 1. Usajili wa Biashara

Biashara inaweza kumilikiwa na mtu binafsi au kupitia umiliki wa biashara kisheria kama vile kampuni au shirika. Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutoka Dar es Salaam ana dhamana ya usajili wa biashara kisheria nchini Tanzania. BRELA hutoa hati za kuandikishwa kwa makampuni ya kigeni na makampuni ya ndani na hati za usajili kwa umiliki wa mtu mmoja (Jina la biashara). Usajili wa jina la biashara unaweza kufanyika kupitia matawi ya Chemba ya biashara, viwanda na kilimo (TCCIA) yaliyopo mikoani.

Biashara yoyote lazima isajiliwe na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kupata namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN) na Cheti cha uthibitisho cha mlipa kodi (Tax-clearance certificate). Ili kupata cheti cha utambulisho cha mlipa kodi, mfanya biashara analazimika kulipa kodi ya mapato tarajiwa, kama hana kumbukumbu za mahesabu, TRA watalazimika kumkadiria kiwango cha kodi. Baada ya hapo, biashara italazimika pia kusajiliwa na afisa biashara wa manispaa au wilaya ili kupata leseni ya biashara[1]. Mmiliki wa biashara ni lazima amiliki au akodi sehemu ya kufanyia biashara ili kusajili eneo biashara hiyo inapopatikana. Uhai wa leseni ya biashara ni mwaka mmoja, tarehe itakayotolewa mwaka husika, itaisha tarehe hiyohiyo mwaka unaofuata. Wakulima wanaouza mazao yao shambani hawatakiwi kuwa na leseni ya biashara.

Biashara ambazo si rasmi zilikuwa zikisajiliwa kwa kupewa leseni iliyojulikana kama ***nguvu kazi*** iliyokuwa ikitolewa na mamlaka za serikali za mitaa chini ya Sheria ya Maendeleo ya Rasilimali Watu. Leseni ya ***nguvu kazi*** ilitolewa ili kurasimisha biashara ndogondogo amabazo hazikuwa na sifa ya kupata leseni kubwa. Hata hivyo, sheria ya Biashara ya Mwaka 2013 ilifuta rasmi matumizi ya Leseni ya ***nguvu kazi***. Ofisi za maendeleo ya jamii zinahusika na kusajili wakulima na vikundi vya biashara katika maeneo yao.

Vyama vya Ushirika sharti visajiliwe kupitia Afisa Ushirika wa Wilaya (DCO).

---

[1] Kitengo B cha Makampuni: Wakala wa bima, Migahawa na hotel za kawaida na nyumba za kulala wageni, Madalali, Wakala wa usafiri, Supermarkets, Stoo, Makampuni ya biashara mikoani, Vyama vya ushirika, Wauzaji wa jumla, Wahandisi wa majengo, Wahandisi wa umeme, Wahandisi wa magari, Wahandisi wa civil work contractors, Wataalamu maalumu, Wachapishaji wa vitabu na magazeti, Wauzaji wa vipuli na vifaa vya mashine, Madalali, Wasafirishaji wa abiria katika majiji, manispaa na miji, Watengenezaji na wauzaji wa bidhaa ndogondogo, Wahudumu wa huduma za simu. Biashara zingine zote zilizosajiliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

**Jedwali 1:** Mwenekano wa jumla wa hatua za usajili wa biashara (Kodi zote ni za mwaka 2015).

<table>
<tr><th>Aina ya usajili</th><th>Taratibu zake</th><th>Mda</th></tr>
<tr>
<td>Jina la Biashara<br>BRELA,<br>Anuani ya BRELA; Jengo la USHIRIKA (TFC). Mtaa wa Lumumba.<br>Simu<br>+ 255 222 180 141</td>
<td>Maombi ya Usajili wa Jina la Biashara (Fomu namba 8) yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya barua pepe au kwa kutembelea ofisi za BRELA kwa ajiri ya kuhakiki jina kama linakubalika na halitumiwi na mtu mwingine. Fomu ijazwe na irudishwe baada ya kulipa ada ya usajili ya shilling 6,000 kwa njia ya bank. Jina na cheti cha usajili kitakuwa tayari wiki 1 au 2 tangu kuwasilishwa fomu ya maombi.<br><br>Kwa sasa mchakato wa kutafuta jina kama linafaa na pia kusajili jina la biashara unaweza kufanywa kwa njia ya mtandano kupitia tovuti ya BRELA, yaani www.brela-tz.org</td>
<td>Wiki 1-2</td>
</tr>
<tr>
<td>Kuandikisha Kampuni<br>BRELA</td>
<td>Mwombaji anatakiwa kuandaa hati za kuanzisha kampuni (memorandum and articles of association) na kuwasilisha BRELA anapoomba kuandikisha kampuni (Fomu 1). Si lazima kutumia mwanasheria japo ni kawaida kufanya hivyo. Ada za ujazaji wa nyaraka zote ni 45,000Tsh.<br><br>Ada za usajili:
<table>
<tr><th>Namba</th><th>Makampuni ambayo hisa zake za mitaji ni:</th><th>Gharama TZS</th></tr>
<tr><td>1</td><td>Zaidi ya TZS 20,000/= na isiyozidi 500,000</td><td>50,000</td></tr>
<tr><td>2</td><td>Zaidi ya TZS 500,000/= na isiyozidi 1,000,000</td><td>80,000</td></tr>
<tr><td>3</td><td>Zaidi ya TZS 1,000,000/= na isiyozidi 2,000,000</td><td>100,000</td></tr>
<tr><td>4</td><td>Zaidi ya TZS 2,000,000/= na isiyozidi 3,000,000</td><td>120,000</td></tr>
<tr><td>5</td><td>Zaidi ya TZS 3,000,000/= na isiyozidi 5,000,000</td><td>150,000</td></tr>
<tr><td>6</td><td>Zaidi ya TZS 5,000,000/= na isiyozidi 10,000,000</td><td>180,000</td></tr>
<tr><td>7</td><td>Zaidi ya TZS 10,000,000/= na isiyozidi 30,000,000</td><td>200,000</td></tr>
<tr><td>8</td><td>Zaidi ya TZS 30,000,000/=</td><td>300,000</td></tr>
</table>
<br>Angalizo; Makampuni yote yaliyosajiliwa yanatakiwa kuwasilisha faida ya mahesabu yaliokaguliwa BRELA amabayo hujazwa katika fomu maalmu. Faida/hasara na mizania ya hesabu ni sehemu ya mahesabu inayowasilishwa BRELA</td>
<td>Baada ya kujaza fomu, kwa kawaida Hati ya Kuandikishwa huandaliwa ndani ya siku 2-3 kama nyaraka zote zipo sawa.<br><br>Hivi sasa BRELA wameanzisha mfumo wa kielectronic wa majaribio ili kupunguza mda wa kusajili majina ya kampuni kwa masaa 8.</td>
</tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| **Usajili** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). | Omba **Nambari ya Utambulisho wa Mlipa Kodi** (TIN) na Hati ya Utambulisho wa mlipa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hutolewa bure kabisa. Wakati wa kuomba nambari ya utambulisho wa mlipa kodi ya Kampuni, mwombaji sharti aambatishe nakala ya cheti cha Kuandikishwa Kampuni kutoka BRELA na Hati ya kuanzisha Kampuni.<br><br>Wakurugenzi wote wa Kampuni sharti wafike kwenye ofisi za TRA kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole (biometric data).<br><br>Mwombaji sharti afike mwenyewe kwenye ofisi za TRA kuchukua Hati ya Utambulisho wa Mlipa Kodi.<br>Ili kupata hati ya Utambulisho wa Mlipa Kodi, Kampuni itatakiwa kukisia`mapato yake katika mwaka huo kwa ajili ya makadirio ya kodi kwa upande wa TRA na kuyalipa awali katika mwaka husika.<br><br>Omba Hati ya Kusajiliwa ya Mlipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kama kampuni yako inatarajia kuwa na mapato yanayozidi **Shilingi Milioni 100.** | Siku 2<br><br>Usajili wa VAT huchukua siku 3–5 |
| **Leseni ya Biashara,** Ofisi za Afisa biashara | Omba leseni ya Biashara kutoka ofisi za biashara za manispaa au wilaya, maombi ni bure kabisa.<br><br>Wakati wa kuwasilisha maombi, mwombaji atatakiwa aambatanishe nakala za nyaraka au uthibitisho ufuatao:<br>Hati ya Kuandikishwa Kampuni<br>Hati ya Kuanzisha Kampuni<br>Uthibitisho wa Uraia wa Tanzania<br>Uthibitisho wa kumiliki sehemu ya biashara<br>Nambari ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN)<br>Hati ya Utambulisho wa Mlipa Kodi<br><br>Mwombaji sharti awe na barua ya utambulisho toka serikali ya Kata (WEO), awe na umri usiopungua miaka18 na awe na sehemu ya kufanyia biashara isiohamishika. Leseni ya Biashara inadumu kwa mwaka mmoja.<br><br>**Ada za leseni za biashara kwa Mwaka**<br>**Biashara — Ada ya Leseni**<br>Maghala — 300,000<br>Migahawa mikubwa — 100000<br>Watoa huduma za vyakula — 100,000<br>Hoteli — 200,000<br>Bima — 200,000<br>Wakaguzi — 300,000<br>Wauzai wa mikate — 100,000<br>Wauza thamani — 200,000<br>Mashine za kusaga — 50,000<br>Wauzaji wa mifugo — 250,000 | Siku 1-3 |

| | | |
|---|---|---|
| | Bucha za nyama 80,000<br>Kiosks 60,000<br>Wauza samaki 40,000<br>Migahawa 50,000<br>Wauza pembejeo za kilimo 150,000<br>Supermarkets 500,000<br>Wauzaji wa Jumla 300,000<br>*Chanzo: Mtwara fieldwork, 2015* | |
| **Usajili wa Vywama vya ushirika** | Vyama vya Ushirika sharti visajiliwe kupitia Afisa Ushirika wa Wilaya. Masharti ya usajili ni pamoja na kuwasilisha;<br><br>Nakala iliyothibitishwa, ya muhtasari wa kikao cha kwanza kilichohudhuriwa na Afisa Ushirika wa Wilaya.<br>Nakala nne (4) za Masharti ya chama yanayopendekezwa na chama husika<br>Nakala nne (4) za fomu ya maombi ya kupata kuandikishwa kwa chama cha ushirika<br>Nakala nne (4) za andiko la kuonyesha matarajio ya kufanikiwa kwa chama (upembuzi yakinifu)<br>Nakala nne (4) za muhtasari wa kuomba kuandikishwa chama cha ushirika<br><br>Ikiwa maombi yatakidhi viwango vilivyowekwa, Mrajis wa vyama vya siasa anatoa barua ya utambuzi(usajili wa muda). Barua hii itaruhusu kikundi kufanya shughuli zake za ushirika kwa miaka mitatu (3) kabla ya kukipatia usajili kamili kama chama cha ushirika. Ikiwa kikundi kitashindwa kukidhi masharti, mathalani kushindwa kuwa na idadi ya wanachama wanaotakiwa, barua ile ya utambuzi (usajili wa muda) itafutwa. Endapo Mrajis atakataa kusajili chama, wanachama wana haki ya kukata rufaa kwa waziri mwenye dhamana na masuala ya ushirika ndani ya siku 60. | |
| **Bima ya Wafanyakazi** | Kila mwajiri lazima amsajili mfanyakazi wake na Bima ya wafanyakazi katika Shirika la Bima lolote apendalo. Ili kumsajili mfanyakazi katika Bima ya wafanyakazi, Mwajiri sharti ajaze Fomu ya maombi ya Bima. Fomu hii lazima ijazwe pindi kampuni au shirika linapomwajiri mfanyakazi. Wamiliki wa viwanda pia wanatakiwa kukidhi mahitaji ya Afya na Usalama Sehemu za Kazi (Occupational Health and Safety Act - OSHA). | Siku 1 |
| **Mfuko wa hifadhi ya jamii** | Kila mwajiri katika sekta rasmi lazima asajili wafanyakazi wake katika mojawapo ya mifuko ya lazima ya hifadhi ya jamii kama vile NSSF, GEPF, LAPF, PPF. | Siku 7 |

| | | |
|---|---|---|
| **Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania**<br>Wavuti **www.tfda.or.tz.** | Ni kosa kisheria kuuza, kuhifadhi au kutengeneza chakula na dawa bila kuwa na leseni inayotolewa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania<br>Usajili wa Majengo ya kuzalishia au kuuzia Chakula na dawa una hatua zifuatazo;<br>Wasiliana na wakaguzi wa TFDA waliopo eneo lako (Ofisi za TFDA za kanda, bwana/bibi afya wa wilaya/Afisa mifugo/au mtu yeyote aliyechaguliwa kwa kazi hiyo).<br>Chukua na kusanya fomu ya maombi iliyojazwa kwa ajiri ya usajili wa majengo au sehemu ya kuuzia chakula au dawa kwa mkaguzi husika.<br>Hakikisha majengo yako yamekaguliwa na mkaguzi kutoka Mamlaka ya chakula na dawa.<br>Lipa ada iliyo ainishwa na Mamlaka ya chakula na dawa Tanzania.<br>Ripoti ya ukaguzi itawasilishwa Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa ajili ya kuikagua na kuipitisha.<br>Ikiwa ripoti ya ukaguzi itapitishwa na kukubaliwa, utapata cheti cha usajili kutoka Makao makuu Mamlaka ya Chakula na Dawa au kupitia mkaguzi wa eneo lako.<br>Leseni ya Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania huwa inabadilishwa kila baada mwka mmoja (Mara nyingi ni tar 1 ya mwezi wa Saba kila mwaka). | Siku 3-6 (Kama nakala zote zipo tayari) |

# 2. Kodi/Tozo na Michango

Malipo yanayofanywa ama katika halmashauri za miji au Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

## 2.1 Kodi ya Mapato

Ni kodi inayotozwa kwenye mapato au faida ya mtu binasfi au kikundi kutokana na ajira, shughuli ya biashara au uwekezaji. Kodi hii hutozwa na TRA kwa kati ya asilimia 11 hadi 30 ya jumla ya mapato yote. Ni wajibu wa kila mtu kutunza kumbukumbu za mapato yake kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya mapato na TRA.

Gharama za uwekezaji na uendelezaji ardhi, mashine n.k. zinazoingiwa na mfanyabiashara au mwekezaji zinajumuishwa na kutolewa katika kukokotoa Kodi ya Mapato. Mapato ya mtu binafsi kutokana na mazao ya kilimo hayatazidi Shilingi Milioni Nne (4,000,000) kwa mwaka hayatatozwa kodi.

### *2.2.1 Kodi ya mapato kwa watu binafsi*

Watu binafsi wamegawanywa katika makundi mawili: wafanyabiashara wadogo ambao hawalazimiki kuwa na vitabu vya mahesabu vilivyokaguliwa, na wafanyabiashara wa kati na wakubwa ambao wanatakiwa kutunza vitabu vya mahesabu yaliyokaguliwa. Wafanyabiashara wadogo wanatozwa kodi kwa mfumo wa makadirio, bali wale wa kati na wakubwa wanatozwa kwa misingi ya kuangalia faida kulingana na mahesabu yaliyokaguliwa.

**Jedwali 2.** Viwango vya kodi kwa watu binafsi wakazi kuanzia tarehe 1/7/2015 kwa mujibu wa sheria ya fedha 2015.

| Na | Mapato ya kutozwa kodi kwa mwezi | Kiwango cha kodi |
|---|---|---|
| 1 | Mapato yasiyozidi TZS 170,000 | Hakuna kodi |
| 2 | Mapato yanayozidi TZS 170,000 lakini hayazidi TZS 360,000 | 11% ya kiasi kinachozidi TZS 170,000 |
| 3 | Mapato yanayozidi TZS 360,000 lakini hayazidi TZS 540,000 | TZS 20,900 ongeza 20% ya kiasi kinachozidi TZS 360,000 |
| 4 | Mapato yanayozidi TZS 540,000 lakini hayazidi TZS 720,000 | TZS 56,900 ongeza 25% ya kiasi kinachozidi TZS 540,000 |
| 5 | Mapato yanayozidi TZS 720,000 | TZS 101,900 ongeza 30% ya kiasi kinachozidi TZS 720,000 |

### *2.1.2 Mfumo wa Kodi ya Makadirio*

Huu ni mfumo wa kodi ambapo wafanyabiashara hutozwa kodi kulingana na makadirio ya mzunguko wao wa biashara. Katika mfumo huu, wafanyabiashara hawalazimiki kuandaa na kupeleka vitabu vya mahesabu yao yaliyokaguliwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mauzo kwa mwaka yanatakiwa yasizidi 20 million TZS na yatokane na biashara husika. Kama mapato yametokana na vyanzo vingine vya mapato kama vile ajira, mfumo wa makdirio ya kodi ya mapato hauwezi kutumika. Endapo kutakuwa hakuna kumbukumbu kabisa, kiasi cha mapato kwa mwaka kitakadiriwa kwa kutumia busara na uzoefu wa mwakilishi wa TRA.

Viwango vya kodi kulingana na mauzo au mzunguko wa biashara kwa mwaka vimeorodheshwa katika Jedwali 3 hapo chini.

Mlipa kodi anapaswa kulipa kodi iliyokadiriwa kwa awamu au mikupuo si zaidi ya minne, katika vipindi vya **miezi mitatu mitatu**. Tarehe za malipo ni kama zifuatavyo; tarehe 31 Machi, tarehe 30 Juni, tarehe 30 Septemba na tarehe 31 Disemba.

**Jedwali 3:** Viwango vya kodi kwa wafanyabiashara wadogo wakazi kuanzia tarehe 1/7/2015 kwa mujibu wa sharia ya fedha ya mwaka 2014.

| **Mauzo kwa mwaka** | **Uzingatiaji wa kifungu cha 80 cha Sheria ya Kodi ya Mapato (Utunzaji wa kumbukumbu)** | |
|---|---|---|
| | **Hakijazingatiwa** (Kumbukumbu zisizoridhisha) | **Kimezingatiwa** (Kumbukumbu zinazoridhisha) |
| Mauzo yasiozidi sh. 4,000,000 | Hakuna kodi | Hakuna kodi |
| Mauzo yanayozidi sh. 4,000,000 na yasiyozidi sh. 7,500,000 | TZS 150,000 | Asilimia 3 ya mauzo yanayozidi TZS 4,000,000 |
| Mauzo yanayozidi sh. 7,500,000 na yasiyozidi sh. 11,500,000 | TZS 318,000 | TZS 135,000 jumlisha asilimia 3.8 ya mauzo yanayozidi TZS 7,500,000 |
| Mauzo yanayozidi sh. 11,500,000 na yasiyozid sh. 16,000,000 | TZS 546,000 | TZS 285,000 jumlisha asilimia 4.5 ya mauzo yanayozidi 11,500,000 |
| Mauzo yanayozidi sh. 16,000,000 lakini hayazidi Shilingi 20,000,000 | TZS 862,500 | TZS 487,000 jumlisha asilimia 5.3 ya mauzo yanayozidi 16,000,000 |
| Mauzo yanayozidi sh 20,000,000 | Ni lazima kutengeneza hesabu na kodi itatozwa kutegemea kiasi cha faida | |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2015

### *2.1.3 Kodi ya mapato kwa wanotunza vitabu vya hesabu zilizokaguliwa*

Hili ni kundi la walipa kodi ambao mauzo yao yanazidi 20,000,000TZS na wanatakiwa kuandaa vitabu vya mahesabu vilivyokaguliwa. Wafanyabiashara katika kundi hili wanatozwa kodi kulingana na faida wanayopata baada ya kutoa gharama za uendeshaji n.k. na sio mauzo.

**Jedwali la 4:** Viwango vya kodi kwa wafanya biashara wanaotunza vitabu vya hesabu zilizokaguliwa

| **Mapato ya kutozwa kodi kwa mwaka** | **Kiwango cha kodi** |
|---|---|
| Mapato yasiyozidi TZS 2,040,000 | Hakuna kodi |
| Mapato yanayozidi TZS 2,040,000 lakini hayazidi Sh. 4,320,000 | 11% ya kiasi kinachozidi TZS 2,040,000 |
| Mapato yanayozidi TZS 4,320,000 lakini hayazidi TZS 6,480,000 | TZS 250,800 ongeza 20 % ya kiasi kinachozidi 4,320,000 |
| Mapato yanayozidi TZS 6,480,000 lakini hayazidi TZS 8,640,000 | TZS 682,800 ongeza 25 % ya kiasi kinachozidi 6,480,000 |
| Mapato yanayozidi TZS 8,640,000 | TZS 1,222,800 ongeza 30 % ya kiasi kinachozidi 8,640,000 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2015

## 2.2 Kodi ya Makampuni

Kodi ya Kampuni hutozwa kwenye faida ya kampuni au shirika inayopaswa kutozwa kodi kutokana na mahesabu ya mwaka yaliyokaguliwa. Kila kampuni iliyosajiliwa au mtu binafsi ambaye anatakiwa kuandaa vitabu vya mahesabu anapaswa kuwasilisha TRA taarifa za fedha zinazoonyesha kiasi cha kodi inayostahili kulipwa katika mwaka husika.

Malipo ya muhula wa kwanza hufanyika wakati wa kuwasilisha makadirio ya awali, na malipo mengine hufanyika kulingana na tarehe zilizotajwa hapo juu.

Kiwango cha kodi ya makampuni nchini Tanzania ni asilimia 30 kwa makampuni binafsi na asilimia 25 kwa makampuni yaliyoorodheshwa katika soko la hisa la Dar es salaam (DSE).

## 2.3 Kodi ya majengo

Kodi ya Majengo hupaswa kulipwa na mtu yeyote anayemiliki jengo, iwe kwa ajili ya makazi au matumizi ya biashara. Kdodi hii hulipwa manispaa au halmashauri za miji. Kiwango cha kodi kinachotozwa kinatumiwa kwa mujibu wa ukubwa, matumizi na mahali jingo lilipo.

## 2.4 Kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

Kodi hii hutozwa kwa mauzo ya bidhaa na huduma inayozidi Million 100 TZS. Kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani ni asilimia 18 ya thamani ya mauzo na hulipwa kwa kamishina wa kodi za ndani TRA.

Chakula; mazao na wauzaji wa mifugo; chakula na dawa za mifugo; dawa za kuua wadudu; mbolea; nyumba za makazi, na ardhi havitozwi VAT.

## 2.5 Kodi ya huduma

Taasisi yoyote iliyosajiliwa inapaswa, kwa mujibu wa sheria kulipa Kodi ya Huduma ya asilimia 0.3 ya mapato yake ya mwaka katika manispaa au halimashauri ya mji husika.

## 2.6 Kodi ya mandeleo ya ufundi TRA

Kodi hii hutozwa kwa kampuni au mtu yeyote aliyeajiri wafanyakazi zaidi ya wanne. Kiwango cha kodi ni asilimia 5 ya kipato cha mfanyakazi.

## 2.7 Kodi ya zuio

Kodi hii kutozwa kwa watoa huduma katika sekta mbalimabli za serikali na binafsi. Kwa watoa huduma kataka taasisi za serikali kama mashule, hospitali n.k kodi ya zuio ni asilimia 2 ya malipo anayostahiki kupata.

## 2.8 Ushuru wa soko

Mtu yeyote anayetaka kuuza bidhaa zake katika masoko yaliyo chini ya halmashauri anapaswa kulipa ushuru wa soko kulingana na aina ya mazao anayouza, iwe kwa reja reja au kwa jumla kama ilivyoolezeshwa hapo chini.

**Jedwali 5:** Ushuru wa Soko (Mtwara, kwa Shilingi)

| Na | Aina ya mazao (na ujazo wake) | Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Nyanya (tenga) | 500 |
| 2 | Maharage (kilo 100) | 1,000 |
| 3 | Mikunde (kunde, mbaazi na karanga) (kilo 100) | 400 |
| 4 | Viazi (kilo 100) | 1,000 |
| 5 | Vitunguu (kilo 100) | 1,500 |
| 6 | Karanga (kilo 100) | 1,000 |
| 7 | Mahindi (kilo 100) | 500 |
| 8 | Ndizi (tenga) | 500 |
| 9 | Mihogo (tenga) | 500 |
| 10 | Kabichi (moja) | 100 |
| 11 | Nanasi (moja) | 50 |
| 12 | Nazi (tenga) | 200 |
| 13 | Pilipili (tenga) | 1,000 |
| 14 | Machungwa (tani moja) | 5,000 |
| 15 | Maembe (tani moja) | 5,000 |
| 16 | Mazao mengine | 200 |
| 17 | Biashara ya reja reja | 200 |
| 18 | Kutumia majengo ya soko (kwa mwezi) | 6,000 |

Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, 2014

## 2.9 Ushuru wa mazao wa serikali za mitaa

Kiwango cha ushuru wa mazao kinachotozwa kwa wanunuzi wa mazao kinatofautiana baina ya wilaya na wilaya, kati ya asilimia 3 had 5 ya bei ya kununua mazao yanapotoka shambani. Ushuru huu hugawanywa miongoni mwa mamlaka mbalimbali za serikali-Kiasi cha asilimia 20 hurudi kwa wakusanyaji wa mapato (Halmashauri za vijiji) na asilimia 80% inakwenda ngazi ya Wilaya.

Mnunuzi binafsi wa mazao lazima awe na kibali cha manunuzi na usafirishaji mazao PDN (Procurement Delivery Note) Kutoka chama cha msingi cha ushirika kilichopo mahali husika ili aruhusiwe kusafirisha mazao nje ya wilaya husika. Kila chama cha msingi kina kiwango cha ushuru kilichopangwa kwa kilo ya mazao yanaayonunuliwa ambacho hutofautiana baina ya wilaya na wilaya, mara nyingi ni kati ya 20-40 TZS/kilo.

Michango mingine inayotakiwa kulipwa na mfanyakazi husika ni pamoja na michango ya shule, hospitali na ujenzi wa barabara. Michango hupangwa na mabaraza ya vijiji.

# 3. Viwango vya Ubora vinavyo-husiana na Usindikaji na uuzaji wa vyakula

## 3.1 Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)

Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) ina mamlaka ya kusajili vyakula vilivyosindikwa, kudhibiti ubora na usalama wa chakula na dawa na kuthibitisha na kusajili majengo yanayotumika kuzalisha au kuuza chakula au dawa hizo. Ni kosa kisheria kuuza, kuhifadhi au kutengeneza chakula, dawa au vifaa tiba bila kusajili jengo linalotumika kwa shughuli hizo kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa au bila ya mzalishaji kumiliki leseni ya bidhaa hiyo toka Mamlaka ya chakula na dawa Tanzania. Hati ya Usajili ya TFDA hutolewa kwa mtu yeyote anayekusudia kuendesha biashara ya chakula na dawa kwa matumizi ya binadamu. Leseni hii hukatwa kila mwaka

**Jedwali 5:** Gharama za TFDA (TZS)

| Aina ya biashara/Ukbwa | Gharama ya usajili na Kibali | Gharama ya ukaguzi |
|---|---|---|
| Maduka ya rejareja | 20,000 | 30,000 |
| Mashine za kusaga/kukoboa | 20,000 | 30,000 |
| Wauzaji wa jumla | 40,000 | 30,000 |
| Hoteli(zenye baa, migahawa) | 40,000 | 30,000 |

*Angalia Jedwali 1 kwa hatua za usajili.*

## 3.2 *Shirika la Viwango Tanzania (TBS)*

TBS inatoa viwango vya kitaifa vya ubora wa chakula na bidhaa zingine zinazouzwa katika masoko ambavyo vinatakiwa kufuatwa. Bidhaa inaweza kujaribiwa kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na kupewa cheti na nembo ya ubora ya TBS ikiwa itakidhi viwango hivyo. Cheti hutolewa mara moja tu, ila bidhaa ikithibitishwa inapaswa kupelekwa sampuli TBS mara kwa mara kwa ajili ya ukaguzi. TBS hufanya ukaguzi mara nne kwa mwaka sehemu ya uzalishaji wa bidhaa husika na ukaguzi huu hufanyika bila kumtaarifu mzalishaji. Ada za cheti cha ubora, nembo na taarifa zingine kuhusu TBS zinaweza kupatikana katika anuani ifuatayo:

Kwa Wajasiriamali wadogo, cheti cha TBS hutolewa kwa mda wa mwaka mmoja bure lakini sharti mtu huyo apitie ofisi za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo-SIDO zilizopo mikoani. Pia anapaswa kutuma sampuli ya bidhaa zilizothibitishwa na TBS mara kwa mara ili kuangalia ubora.

TBS, Ubungo, Barabara ya Morogoro / Sam Nujoma , S.L.P 9524, Dar es Salaam, Simu.: +255 22 245 0298 | +255 22 245 0206, Nukushi: +255 22 245 0959, Tovuti: info@tbstz.org

# 4. Usajili wa Maghala

Ghala lolote ambalo linatumika katika mfumo rasmi wa Stakabadhi Ghalani (Mkopo kwa dhamana ya bidhaa) lazima liwe limesajiliwa na Bodi ya Leseni ya Maghala Tanzania (Tanzania Warehousing Licensing Board- TWLB). Mwombaji atatakiwa kujaza Fomu Namba 1. Bodi ya Maghala imepewa mamlaka ya kukagua na kusajili au kutoa leseni kwa maghala yote yaliyo katika mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Leseni hii huitwa "Leseni ya Biashara ya Maghala." Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unaweza kutumiwa na watu binafsi kibiashara. Kwa mikoa ya Lindi na Mtwara mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani hutumika kisheria kwa zao la korosho na ufuta.

TWLB, NIC Kitegauchumi, Horofa ya 12, Wing "B" , Mtaa wa Samora S.L.P. 38093, Dar es-Salaam, Simu: +255 552 128 691, Nukushi: +255 222 128 692, Tovuti: twlbwrs@gmail.com, info@wrs.go.tz

# 5. Usajili wa Vyombo vya Usafirishaji

Mamlaka ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA), inawataka waendeshaji/wamiliki wa magari yenye uzito wa kuanzia tani 3, kusajiliwa na SUMATRA. Wakati wa usajili waendeshaji/wamiliki watatakiwa kutoa taarifa/vielelezo vifuatavyo:

1. Maelezo binafsi ya mwendeshaji, mmiliki au kampuni
2. Taarifa kuhusu chombo (gari) husika (ikiambatana na nakala ya kadi ya usajili wa gari)
3. Aina ya shughuli/biashara
4. Gharama ya kukodi kwa tani-kilomita, au kwa namna yoyote inayotumika kukokotoa tozo ya usafirishaji/nauli
5. Nakala ya Hati ya Bima iliyo hai
6. Hati ya Ukaguzi wa Gari kutoka Polisi (VIR) pamoja na stakabadhi ya malipo ya hati ya ukaguzi
7. Nakala ya Leseni ya Dereva, picha pamoja na mkataba wa ajira ulioridhiwa na wizara ya kazi
8. Ratiba pamoja na sampuli ya tiketi

Fomu za kujaza taarifa zinazotakiwa zinatolewa bure katika ofisi za SUMATRA kwa anuani hapo chini, na pia zaweza kupatikana katika tovuti ya SUMATRA (www.sumatra.or.tz) Kwa wilaya zilizo mbali na makao makuu ya mikoa, fomu hizi zawezapatikana kwenye ofisi za Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya. Vivyo hivyo, leseni zitatolewa kwa kila gari linalouzwa. Waombaji/wamiliki hutakiwa kuchangia Shilingi 5,000 tu kwa ajili ya kuandaa leseni na gharama za kiutawala

SUMATRA Mtwara S.L.P 925, Simu. +255 23 233 3179, Simu: +255 758 807 753 na Lindi S.L.P 727, Simu: 023-2202914

# 6. Masuala Mengine ya Kisheria Kilimo

## 6.1 Kilimo cha Mkataba

Kilimo cha mkataba kinatambuliwa kisheria kwa mazao ya korosho na mazao mchanganyiko (Sheria Na 18 ya Sekta ya Korosho ya mwaka 2009, Kifungu cha 14 na Sheria Na 19 ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya mwaka 2009, Kifungu cha 16). Hata hivyo, kilimo cha mkataba cha Korosho sharti kiridhiwe na kudhibitiwa na Bodi ya Korosho.

## 6.2 Pembejeo za Kilimo

Ni marufuku kuuza mbegu ambayo haijakaguliwa na kuthibitishwa na Wakala wa Udhibiti wa Mbegu Tanzania (TOSCI). Ni marufuku mtu yeyote kuuza au kusambaza mbolea iliyochakachuliwa, au mbolea au virutubisho vya mbolea vilivyo chini ya kiwango. Viatilifu vyote lazima vithibitishwe na Taasisi ya Utafiti wa Viatilifu vya Kitropiki (TPRI). Ni kosa kwa mtu yeyote atakayetengeneza kemikali, kuagiza, kusambaza, kuuza au kutangaza bidhaa za sumu za wadudu mbali na zile zilizosajiliwa, na kwamba mtu huyo atakabiliwa na faini au kifungo gerezani au vyote kwa pamoja.

## 6.3 Vibali vya Usafirishaji Mazao na Mifugo

Ili kusafirisha mazao nje ya wilaya, mnunuzi anatakiwa awe na kibali cha kununua na kusafirisha mazao PDN (Procurement Delivery Note) kutoka katika Chama cha msingi cha mahali aliponunulia mzigo.

Kusafirisha mifugo kutoka sehemu moja kwenda nyingine nchini ni lazima kuwa na kibali. Wizara inayohusika na jambo hili ni Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, kupitia Kurugenzi ya Huduma ya Tiba za Mifugo (Veterinary Service Division - VSD). Kurugenzi ya Huduma ya Tiba ya Mifugo inazo ofisi za kanda. Kwa Kanda ya Kusini, ofisi ziko kituo cha utafiti Naliendele (NARI). Msafirishaji aliye na stakabadhi ya malipo kutoka kwenye Kituo cha Huduma ya Tiba ya Mifugo (Veterinary Investigation Centre, VIC) hupatiwa kibali chake kutoka kwa Afisa Mifugo wa Wilaya husika.

Meneja wa kliniki ya mifugo Naliendele-NARI, 0732333218

## 6.4 Wakala wa Vipimo (WMA)

Wakala wa vipimo wana mamlaka ya kudhibiti vifaa vyote vinavyotumika katiaka upimaji kama vile Mizani, pampu za mafuta n.k. Pia Wakala wa vipimo hufuatilia mienendp ya upimaji katika maeneo mbalimbli ili kubaini kama kuna usahihi au la kwa njia ya kaguzi za dharura. Uhakiki wa vipimo hufanywa kila mwaka. Mara nyingi mkaguzi hutembelea makao makuu ya wilaya, na kata na kisha kuwaomba wafanya biashsara kupeleka mizani zao zote kwa ajiri ya uhakiki. Uhakiki unaweza pia kufanya katika ofisia husika ya Wakala wa vipimo.

## 6.5 Mahitaji ya ufungshaji wa bidhaa kwa mujibu wa Wakala Wa Vipimo

- Alama za Utambulisho wa Bidhaa.
- Jina na mahala bidhaa ilipozalishwa, mfungashaji, msambazaji, muingizaji inchini na muuzaji wa reja reja.
- Idadi sahihi ya bidhaa.
- Kipimo kinachutumika kielezwe kwa alama au maneno i.e. Kg au Kilo, g au gramu etc.
- Alama zote zitumie lugha ya taifa.

Wakala wa vipimo, Horofa ya 4, Mwalimu House, Mtaa wa Uhuru S.L.P 313, Dar es-salaam, Simu +255 22 2203199, Nukushi +255 22 2203200, tovuti: *info@wma.go.tz.*

Ofisi za Mtwara 0717 479 433 (Meneja), 0717 098 719 (Afisa Vipimo), 0787 178 266 (Wakala wa vipimo)

## 6.6 *Vikwazo vya Biashara visivyo* vya Ushuru (NTB)

Shirikisho la wenye Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), kwa kushirikiana na shirika la Trademark East *Africa*, *pamoja na* wizara ya viwanda na biashna na taasisi mbalimbali za serikali, linaendesha mfumo wa simu za mkononi kwa ajili ya kutolea taarifa za matatizo yanayotokana na Vikwazo vya Biashara visivyo vya Ushuru (NTB). Utaratibu wa kutoa taarifa ni kama ifuatavyo:

1. Andika **NTB** kisha acha nafasi
2. Andika aina ya vikwazo vya biashara visivyo vya ushuru unavyokabiliana navyo
3. Tuma ujumbe (meseji) kwenda 15539
4. Utapokea ujumbe kuwa tatizo lako linashughulikiwa
5. Ujumbe pia utakupatia nambari maalum ya kumbukumbu kwa ajili ya ufuatiliaji

Ili kufuatilia mchakato wa tatizo ulilolitolea taarifa:

1. Andika TAARIFA kisha acha nafasi
2. Andika nambari yako ya kumbukumbu (kutoka 5 hapo juu)
3. Tuma kwa 15539

## 6.7 Sheria za Kazi

Mtu au Kampuni inayotaka kuajiri mfanyakazi inapaswa kuzingatia sheria za ajira ikiwa ni pamoja na kutoa mkataba wa ajira kwa wafanyakazi wake. Muda wa saa za kazi hautakiwi kuzidi saa 9 kwa siku, kwa siku 6 kwa juma. Kiwango cha mshahara hakipaswi kuwa chini ya Shilingi 100,000 kwa mwezi katika sekta ya kilimo, na si chini

ya Shilingi 115,000 kwa mwezi katika viwanda na biashara, bila kujumuisha michango ya lazima ya mwajiri kama vile mchango wa hifadhi ya jamii.

Mwajiri anapaswa kumpatia mtumishi wake likizo isiyopungua siku 28 kwa mwaka; likizo ya uzazi ya siku 84 kwa mwanamke (siku 100 iwapo atajifungua mtoto zaidi ya mmoja), na likizo ya uzazi ya siku 3 kwa mzazi mwanaume, ambayo inapaswa kuchukuliwa ndani ya juma moja tangu mke wa mfanyakazi huyo ajifungue. Mwajiri pia anapaswa kutoa likizo ya ugonjwa kwa wafanyakazi wake ya siku 126. Katika siku 63 za kwanza mfanyakazi anastahili kulipwa mshahara kamili na katika siku 63 zinazofuata anastahili kulipwa nusu mshahara. Kabla ya kuchukua likizo ya ugonjwa, mfanya kazi anapaswa kuwasilisha kwa mwajiri uthibitisho wa Daktari.

Mwajiri pia anapaswa kuzingatia kanuni za kumwachisha kazi mtumishi. Kutozingatia hilo kunasababisha kuachishwa kazi kusiko fuata haki, Kutozingatia kanuni na taratibu husika kutasababisha mtumishi aliyeachishwa kazi kurejeshwa kazini au kulipwa fidia. Mwajiri anatakiwa kumsajili mfanyakazi katika mifuko ya mafao ya kazi kwa chaguo la mfanyakazi na kuwa na bima ya kazi.